

Wavuvi haramu waendelea kukamatwa

Na Mwandishi Wetu, Arusha

UONGOZI wa Hifadhi ya Ziwa Duluti chini ya Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) umesema unaendelea kukamata wavuvi haramu kwenye Ziwa hilo, kwa kuwa uvuvi wanaofanya ni haramu.

Hayo yalielezwa juzi na Mhifadhi Misitu Mwandamizi, Peter Muyonga akizungumza na vyombo vya habari kuhusu Hifadhi hiyo.

Muyonga alisema bado kuna changamoto usiku kwa wananchi wanaoishi karibu na Ziwa hilo kuvua, jambo ambalo ni hatari kwani hakuna mwananchi anayeruhusiwa kuvua.

Alisema miaka ya nyuma kidogo, kulikuwa na tatizo hilo, lakini limepungua ingawa bado wanaoendeza uvuvi haramu wanakamatwa.

"Tumeweka mikakati ya kubaini watu hawa wanaotumia ujanja kuvua samaki kiharamu, hatutawaacha salama, oparesheni kadhaa zilishafanyika na tunaziendeza, tukumbuke tu huu ni urithi kwa vizazi vijavyo," aliongeza.

Pia, aliwataka wananchi wanaouziwa samaki wanaovuliwa na wavuvi haramu kuacha kuwanunua na badala yake wawe mabalozi wazuri wa kutangaza uzuri wa Ziwa hilo ambalo ni kivutio cha utalii.

Alisema idadi ya watalii imeongezeka kwa kasi huku ongezeko hilo likijumuisha watalii wa ndani tofauti na miaka iliyopita. Alitolea mfano kuwa katika miaka ya 2016 na 2017 watalii wa ndani walikuwa 3,400 huku wa nje wakiwa 5,260 na sasa idadi ya Watanzania wanatembelea hifadhi hiyo imeongezeka.

Alisema lengo halisi ni kuhakikisha watalii wa ndani wanazidi 5,000 jambo linalowezekana kwa kuwa hifadhi ya Ziwa hilo ni kwa ajili ya kuenzi utalii.

...uu wa Serikali zianze

...uu kujisanuhisha na ku-torejea makosa ya nyuma,

mazito wanayoyatekeleza, jukwaa hili litufanya tuwe

Wizara yatangaza wiki ya mifugo, yazindua kituo

Na Frank Leonard, Iringa

WIZARA ya Mifugo na Uvuvi imezindua kituo cha Wakala wa Maabara ya Huduma za Mifugo (TLVA) mjini Iringa huku ikitangaza kuanzisha wiki ya mifugo itakayo-adhimishwa kila mwaka kuanzia mwaka ujao wa fedha.

Uzinduzi wa kituo hicho kitakachohudumia wafugaji wote wa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini umekwenda sambamba na maadhisho

ya wiki maalumu ya wakala hiyo katika kusherehekeea miaka 10 ya kuanzishwa kwake.

Akizindua kituo hicho, Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Mifugo), Tixon Nzunda aliwataka viongozi wa mikoa hiyo kuhamasisha wananchi na wafugaji kutumia huduma hizo za kiveterinari ili waiboreshe mifugo yao na kukuza uchumi wao na taifa kwa ujumla.

"Huu ni wakati wa kufuga kisayansi na ndio maana tumewaletea kituo

hiki ili kiwasaidie kutekeleza shughuli zenu za ufugaji kisasa kwa kuzingatia mab-adiliko ya teknolojia kupitia mfumo mpya wa kidijitali wa kusajili viuutilifu vya mifugo, ufuutiliaji, uzalishaji na usambazaji wa chanjo unaotumiwa na TVLA," alisema.

Kwa upande wake Mtendaji Mkuu wa wakala hiyo, Dk Stella Bitanyi alizungumzia mafanikio ya wakala hiyo nchini kuwa ni pamoja na kuongezeka kwa vituo vyake kutoka viwili hadi 13 ndani ya miaka 10.